# Jarida la UQAB

**Toleo 2**
**Machi 2017 MILADI**
**Jumadu Thani 1438 AH**

Kifo Cha Mlinganizi wa Kiislamu


Hali ilivyo nchini Somalia

Kukumbatia Urasilimali

Tatizo la Ajira



## Jeshi la Polisi Laifanya Kenya Nchi YaKimabavu



# Tangazo la Kifo cha mmoja wa walinganizi wa Kiislamu Kenya: Ahmed Swaleh Al Amry ( Mola amrehemu)

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kwa nyoyo zenye kuamini Qadhaa ya Mwenyezi-Mungu na Qadar yake harakati ya Kiislamu ya Hizb ut-Tahrir Kenya, inawatangazia umma wa Kiislamu wote kwa ujumla na hasa Waislamu nchini kenya kifo cha mbebaji shupavu wa ulinganizi wa haki wa kuregesha maisha ya Kiislamu kupitia kuisimamisha tena Khilafah kwa manhaj ya Mtume (saw); Ustadh Ahmed Swaleh Al Amry. Marhum alipatwa na mauti saa tatu asubuhi Jumane tarehe 31 Januari 2017 sawa na 03 Jumadal 1 1438 AH.

Mbali na kuwa mwanachama wa Hizb ut-Tahrir, Ndugu yetu Ahmed Allah amrehemu alikuwa msimamizi wa tuvuti ya Hizb ut-Tahrir kanda ya Afrika Mashariki kwa zaidi ya mwongo mmoja.Tulimjua kwa ikhlas yake na kushuhudia bidii yake katika kubeba daawah tukufu ya Kiislamu na wala hatusifu yoyote mbele ya MwenyeziMungu.

Tunaipa pole familia ya marhum na kuiombea kwa Allah awape moyo wenye kusubiri na kuwalipa kwa ujira wao in shaa Allah wakati huu wa huzuni.Nasi hatuna la kusema ila lile analoridhia Mola wetu nalo ni

{ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعونَ }

**“Hakika sisi ni wa MwenyeziMungu na kwake yeye ni wenye kuregea”** [al-Baqara:156]

Kwa hakika nyoyo zetu zimejaa huzuni na macho yakitoa machozi kwa kuondokewa na ndugu yetu, twamuomba Mola amsamehe na kumrehemu na kumweka mahala pema peponi. Ewe Allah twakuomba ukirimu mashukio yake na kukunjua kaburi lake na umpe nyumba bora zaidi kuliko aliyokuwa nayo duniani nasi tukawe naye chini ya bendera ya Mtume (saw) siku ya Qiyama.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Jeshi la Polisi Laifanya Kenya kuwa Nchi ya Kimabavu



Tarehe 16 Januari, 2017, Raisi Uhuru Kenyatta alizindua zaidi ya magari 500 ya polisi hii ikiwa ni muendelezo wa mipango ya kuiboresha idara ya polisi kwa vifaa vya kisasa. Vyombo vya habari vya kitaifa na mataifa waliangazia tukio hilo kwa sura ya mkato na kushindwa kutathmini kwa kina lengo la mpango huo. Hapa tunatoa tathmini ya kina ya kuhusu mipango hiyo ya kuifanya idara ya polisi kuwa ya kijeshi.

Upofu wa kijamii na kiitikadi ya wanafikra kutoka eneo la Afrika hauwazuii wao kuisitisha katiba na utekelezwaji wake kupitia sharia za kijeshi ambazo zimeidhinishwa na kipengee cha kupambana na ugaidi cha Prevention of Terrorism Act 2012. Udanganyifu wa kuvunja hali ya haki na uadilifu hakukuanza na Raisi Uhuru Kenyatta 16 Januari, 2017 kutoa agizo la kupambana na wachochezi 'kikatili', bali ilianza kitambo mno kupitia njama ambazo hakuna hata moja aliyejali kuzificha.

**Sheria ya Kijeshi ya Lazima:** Aliyekuwa Jaji mkuu Willy Mutunga katika hatamu yake alinena kwa vyombo vya habari kuwa aliitisha mkutano kati ya Mahakama na Vitengo vya Kiusalama tarehe 29 Mei, 2014, ambao ulihudhuriwa na Usimamizi wote wa Usalama wa Taifa, Waziri wa Usalama wa Ndani na Ulinzi, Inspekta wa Polisi, Mkuu wa Jeshi Kenya (KDF), Mkurugenzi Mkuu wa Kitaifa wa Ujasusi na wawakilishi kutoka katika Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

Alifichua "Mkutano huo ulikuwa ni kilele cha mazungumzo kati yake na vitengo tofauti vya usalama ambayo yalikuwa yakiendelea kwa miaka miwili. Mikutano hii ilikuwa juu ya msingi wa kufahamu kwamba tunapokuja katika masuala ya usalama na ustawi wa raia, lazima nguzo tatu za serikali ziratibu na zishirikiane kwa karibu." Aliendelea kusema kuwa yeye kama mwanasheria ametambua kuwa kuna mgongano wa wazi katika nukta muhimu za 'Kugawanywa kwa Mamlaka' akisema "Ingawa vitengo tofauti vya Serikali viko huru, Katiba inavitaka vitegemeane." Akiandaa mazingira ya kusitisha katiba kwa kusema paruwanja, "Ugaidi ni vita visivyotumia njia zakawaida…sisi lazima tuwe wabunifu ili kupambana na vita hivi."

Angalizo,**sio Katiba, bali "Ubunifu".** Hapo awali 26 Mei, 2014; Cyrus Ombati, mwanahabariwa Gazeti la The Stanadard alimnukuu Makamu wa Raisi William Ruto akiwashtumu mahakimu na majaji kwa kuwaachilia washukiwa wa ugaidi kwa dhamana eti inaregesha nyuma vita dhidi ya ugaidi akisema "tunatoa wito kwa washikadau wote katika idara ya mahakama kusimama na waKenya".

Angalizo,**sio Pamoja na Sheria.** Jaji Mkuu Willy Mutunga, alikiri kuwa alikuwa chini ya msukumo mkubwa kuisitisha Katiba. Kukiri huku kutoka kwa Mwenyekiti wa nguzo ya Mahakama kungetoa onyo lakini tunaishi katika zama za ujinga na kutojali bahari za habari. Hatimaye Jaji Mkuu alizidiwa na kubuni timu itakayotathmini masharti ya dhamana kwa wale walioshtakiwa chini ya Kipengee cha Sheria cha Kuzuia Ugaidi.

Mwenzie katika nguzo ya Utendaji – Mwanasheria Mkuu Githu Muigai, anajulikana kuwa karibu na walioko mamlakani na msaliti wa Vyama vya Kiraia, mwaka 2014 mara tofauti alipendekeza kuweka sharia za kudhibiti taasisi za dini na mitandao ya kijamii; akifuata viashirio vya mabepari katika kudhibiti mitandao ya kijamii. Mapendekezo yake yalikuja siku 7 baada ya Theresa May wakati alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani alipotangaza pendekezo maarufu la kuwalazimisha wamiliki wa huduma za mitando wazi na makampuni ya huduma za simu kuweka rekodi za watumizi za mitandao hiyo na simu hizo; pendekezo hilo lilipita. Akijaribu kuituliza jamii ya Wakristo, alifichua kuwa Wakristo sio walengwa na sharia zilizopendekezwa bali ni "vikundi vidogo vinavyo wadanganya wafuasi na kushiriki katika misimamo mikali na mafundisho mengine hatari" kiujanja akiwalenga Waislamu. Kwa bahati, viongozi wa makanisa walifahamu kuweko kwa sharia hiyo itakuwa ni muda mchache tu itakapotumika dhidi yao pia na wakashikilia msimamo wao; na kwa mara nyingine sio ya kwanza katika historia ya Waislamu kuokolewa na Wakristo na nidhamu isiyotambua muumba (juu ya kuwa sio makusudio yenyewe).

*Endelea Uk..4*

Kwa vitendo na matamshi ya kisiasa utaratibu wa katiba ukaharibiwa kiasi kwamba Serikali ikafeli kitaalamu na kupelekea Rais Barack Obama kuwakasirisha wapambe wanatumia wa mtandao wa kijamii wa Twitter walo ughaibuni, kwa kupiga kelele kuwa "Mfalme yuko Uchi" kupitia barua kwa Umoja wa Baraza la Umoja wa Mataifa kuoredhesha mataifa yaliyofeli na kujumuisha Kenya. Wasomi wetu wenye upofu wa kiitikadi walifeli kuelewa ya kua "Haki ya mshtumiwa kupelekwa kotini" ni jambo liloekwa pembeni kwa mda mrefu kwani kina Hemed na vijana wengi walipotezwa na Polisi kutokana na athari yake. Hii ni kutokana na nusu karne ya mipangilio ya kielimu ya mkoloni yalowafanya wanyenyekee na kutwii mamlaka na hili limewadhamini wasomi kutokua na mwamko, wakidhaniwa wema basi waweze japo kudhibiti sharia za uchumi wakutosheleza kuwezesha jumla ya watu kuwa na matumaini yakupata angalau riziki.

**Serikali ya kipolisi ya kimabavu**

Kulingana na kamusi ya elimu za tamaduni, Serikali ya kipolisi ni taifa ambalo viongozi wake hudhibiti nidhamu na utiifu kwa kutumia vitisho vya polisi ama nguvu za kijeshi; kiholela na kiukatili. Kulingana na Wikipedia, ni serikali ambayo hutumia nguvu kiholela kupitia nguvu za polisi.

Kwa vipimo hivi, taifa la Kenya daima limekua ni serikali ya kipolisi ikiwa na viwango tofauti vya dhulma zikitegemea hali za siasa na kiuchumi nchini na kiulimwengu.

Basi kwa nini limekuwa jambo muhimu sasa? Hata hivyo, nchi gani ya Kiafrika haitawaliwi kupitia Serikali ya kipolisi?

**Sehemu mbili**

Nchini,Uvamizi wa faragha binafsi, ama moja kwa moja kimwili au kwa ufuatiliaji(surveilance).
Kimataifa, miangilio iliopo chini ya serikali za kibepari.

Kukua kwa miundombinu ya polisi kitaifa kwa kiwango cha kasi inatishia. Imeenea na kukua kwa wakati zaidi ya muongo moja na kuenea kwa sekta za umma, kibinafsi na nyanja za serikali kuipa uzito kutathmini ukubwa wa hatari wake bila kutia bidi kubwa ya kifikra.

Makala haya ni majaribio ya kuonesha baadhi ya vipengele vyake vinavyodhihirika. Vinavyodhihirika ikimaanisha vile ambavyo ni wazi na vyajulikana na ummah. Mifano ya zile zisizo onekana na itakuwa vigumu kugusia mfano, mikataba ya siri kati ya serikali na ambayo hufichuliwa tu katika hali ya kipekee ya kisiasa kama wakati ripoti iliyotolewa na Kamati ya Upelelezi wa Seneti ya Marekani ikifafanua vyumba vya siri vya CIA vilivyofunguliwa Nairobi au wakati Marekani ilijaribu kupitisha sheria ambayo itailinda shirika la FBI kutokana na kushtakiwa wakati waliuwa raia wa Marekani kinyume na sheria. Kimsingi,"leseni ya kuua" ndani ya nchi ilionekana na kutoweka kutoka kwenye mjadala wa umma.

-Mpango wa Nyumba kumi umewezesha utabikishaji wa vitambulisho vya digitali na athari zake
-Mpango wa jeshi kusimamia Nairobi (Nairobi Metropolitan Command) ukiongozwa na Hon. Aden Duale uliolenga kugeuza Nairobi kuwa chini ya Jeshi.(Katika Historia ya Marekani iliyodhihirishwa Amri ya Raisi Nambari 9066 ya mwaka 1942 iliyosainiwa na Rais Franklin D. Roosevelt kuidhinisha katika hali ya vita, makamanda wa kijeshi kutangaza maeneo ndani ya Marekani kama maeneo ya kijeshi ambayo mtu yeyote anaweza kutengwa . Ilitumika dhidi ya watu wasiokuwa wenyeji wenye asili na adui. Jeshi la Kenya linalofadhiliwa na Marekani na liko katika hali ya vita, linaweza siku moja kwa mfano kuondoa Wasomali wote kutoka Nairobi na kuwafungia katika makambi au gereza kubwa kama serikali ya Marekani alifanya kwa Wajapan wakati huo.)
-Pendekezo la mkuu wa sheira kusimamia taasisi za kidini na mitandao ya kijamii
-Kufanya kikosi cha polisi kiwe na uwezo wa jeshi
-Usambazaji wa vifaa vya kijeshi kwa sura ya vifaru vilivyo angikwa bunduki mashine kwa idara za usalama kudhibiti sheria na nidhamu kwa raiawasio na silaha
-Kuinuka kwa mashirika ya kibinafsi kwa kazi ikichukua majukumu na kazi kiasili zaserikali katika mambo ya usalama na uangalizi wa karibu (mfano hai ikiwa ni mradi wa camera za uangalizi wa safaricom) kufunga mageuzi ya taifa kuwa ni Serikali ya kipolisi ya kimabavu.

Kilele chake ni pale Rais Uhuru Kenyatta alipotangaza February tarehe 16 mipango ya kujenga jela maalum ya "wenye itikadi kali", Guantanamo Bay ya Kenya iliokusudiwa kuzuia "kueneza sumu ya itikadi zao kwa wafungwa wengine" bimaana sehemu kando itakayo watenga na wafungwa wenye fikra tofauti.

Pili,Serikali za kikoloni zimevunja katiba zao huku Marekani ikiongoza njia kupitia Mwanasheria Mkuu wa Marekani Eric Holder alipopitisha ujumbe wa kisheria kumruhusuRais Barack Obama kuua raia wa Marekani na akageuza dunia nzima kuwa uwanja wa vita na kila mwanadamu kuhisi nguvu hii. Sheria ya "Kupambana na Ugaidi na Sheria ya Adhabu ya Kifo ya 1996 (AEDPA)" pamoja na "Hatua Maalum Tawala" zilivunja haki ya kumpeleka mshtakiwa mahakamani (Habeas Corpus). Mapambano yasiyoisha sasa yako kati ya mkono wa Serikali ya Marekani na Mahakama kuhusu kama watuhumiwa au wale wametangazwa kuwa wapiganaji adui hata wakati ni raia wa Marekani lazima wafikishwe mahakamani.

Seriakali za kikoloni pia zilivunja udanganyifu wa Sheria ya Kimataifa, huku ujumbe wa George Bush unaoitwa "Kuonesha huruma kwa wafungwa wa Taliban na Al-Qaeda" na kauli yake kwa umma kwamba wapiganaji maadui hawatakubaliwa ulinzi chini ya Mkataba wa Geneva.

Hii ina athari kwamba nchi kama Kenya haioniumuhimu au motisha ili kudumisha udanganyifu wa Utawala wa Sheria.

Kwa ufupi, vita dhidi ya ugaidi vimepuuzilia mbali kiini macho cha kimataifa kuhususheria. Kama kesi ya Jamhuri ya Kenya Nambari 164/14 "JKIA"

*Endelea Uk..5*


Email: uqab@hizb.or.ke

ambapommiliki wa Pasipoti ya kidiplomasia wakati wa kuandika makala hii anashikiliwa chini ya kifungu cha Kuzuia Ugaidi cha mwaka 2012 ikidhihirisha hakuna sheria hata ya Kimataifa chini ya “Vita dhidi ya ugaidi “. Nidhamu ya mfumo wa kirasilimali imeanguka, na binadamu wote wanatawaliwa na mabwenyenye wasiokuwa na mtazamo wa kiroho kupitia udhalimu wa serikali zinazohifadhiwa na vikundi vya polisi wauaji wenye misimamo ya jeshi.

**Hitimisho**

Ubepari umefeli na kwahilo unafiki wa uhuru na demokrasia pamoja na soko huru umeisha.

Ni upi muelekeo?

Uzalendo ni fungamano la msingi unaolenga kutawala na daima kusababisha vita vya uchokozi kwa vile kila jamii inatia juhudi ili kutawala juu ya wengine. Kama vile Ulaya kupitia vita vya miaka 100 kabla ya utaifa, hali yake baada ya vita vya kwanza vya dunia, vita vya pili vya dunia na Amerika ambaye ni kiongozi wa Demokrasia imekuwa katika vita kwa miaka 214 ya miaka 235 ya kuwepo kwake.

Uzalendo na mitagaa yake yote kama kilimwengu, ushirikiano wa kikanda, ukabila, ukoo hauwezi kuwa ndio msingi wa kujenga amani ya kijamii na kisiasa. Wanadamu lazima wabadilishe msingi wa utaratibu wake wa kijamii na kisiasa kutoka kwa ule wa bandia kama Usekula au Ukomunisti au ule kutoka kwa fungamano la kizalendo kuelekea kwa moja uliyo madhubuti, unayotokana na Muumba wa viumbe na inayoweza kukidhi mahitaji ya binadamu ikitegemeana kwa kila nyanja ili kujenga mtu mwenye busara. Chombo ambacho kitaleta mataifa na tamaduni mbalimbali za ulimwengu pamoja zinazostahiki usimamizi nao ni KHILAFAH.

**Arkanuddin Yassin**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**



# Matatizo Nchini Somalia Hayatotatuliwa Kwa Serikali Za Vibarakala

Uchaguzi wa rais wa Somalia ulifanywa tarehe 8 Februari 2017 katika eneo la Hangar lililoko kwenye uwanja wa ndege wa kimataifa wa Aden Adde mjini Mogadishu. Wabunge nchini humo walimchagua Mohamed Abdullah ‘Farmanjo’ aliyehudumu kama waziri mkuu wa Somalia miaka 2011-2015 ambaye pia ndiye mwanzilishi wa chama cha kisiasa cha Tayo. Katika jumla ya kura zote 328 za Wabunge, Mohamed alishinda kwa kupata kura 184. Kwa kile kilichoelezwa kama mabadiliko ya uongozi kufuatia hatua ya raisi wa sasa Hassan Sheikh Mahmoud kukubali kushindwa pia akampongeza Farmanjo. Uchaguzi huu unatajwa kama hatua ya kufikia kwenye suluhisho la kudumu kwa matatizo sugu yanayoikumba Somalia yakiwemo vita, umasikini na jinamizi la ufisadi.

Taifa la Somalia lililobuniwa na mkoloni Muingereza kama himaya yake na koloni ya Utaliano limegubikwa na vita vya kikabilia na kiukoo ambavyo nyuma ya pazia vina dhaminiwa na wamagharibi. Hii ni kufuatia kupinduliwa kwa dikteta wa kijeshi Meja Jenarali Siad Barre mwaka 1991 aliyetawala taifa hilo kwa miongo miwili. Kwenye mapinduzi hayo chama cha Siad Barre cha Somali Revolutionary Socialist kiliong’olewa kwa utawala na muungano wa makundi ya kijeshi ya upinzani yaliyojumuisha vyama vya Somali Salvation Democratic Front (SSDF), United Somali Congress (USC), Somali National Movement (SNM) na Somali Patriotic Movement (SPM). Kama makundi ya kisiasa yasokuwa ya kisilaha pia yakashiriki kwa mapinduzi hayo.

Baada ya kupinduliwa kwa Barre na kuingia madarakani kwa Ali Mahdi Muhammad ambaye aliweza tu kudhibiti Mji mkuu wa Mogadishu, kuliibuka mapigano baina ya wababe wa koo za Kisomali katika kung’anga’nia Mogadishu. Ali Mahdi alipigana na genarali Mohamed Farah Aidid kwa ajili ya kuzozania madaraka hali iliyofanya vita vya kimbari hasa baina ya wakuu wa koo kubwa za Kisomali kupamba moto zaidi na kupelekea mgawanyiko wa kimajimbo kama vile Jimbo la Somaliland na na lile la Puntland. Hali hii ikapata mvuto wa Kimataifa ambapo Marekani chini ya kile alichokiita misaada ya kibinadamu akatuma wanajeshi 30,000 Somalia kwenye oparesheni ilioitwa Oparesheni Rudisha Matumaini. Operasheni hii ya kijeshi ilidaiwa ni kuleta amani na usalama nchini humo.

Mwaka wa 2006, baada ya muungano wa Mahakama za Kiislamu kuweza kuchukua udhibiti wa Mogadishu na ukaleta utulivu fulani hii ni baada ya muungano huo kutabikisha baadhi ya sheria za MwenyeziMungu (swt). Lakini mwaka mmoja baadae yaani 2007, Jeshi la Ethiopia na lile la muungano wa Afrika likisaidiwa na Marekani yalivamia Somalia kupambana na muungano huo wa mahakama na hatimaye kukabuniwa serikali ya mpito ya Somalia iliyokuwa ikiungwa mkono na Umoja wa Mataifa, Muungano wa nchi za Afrika (AU) na Amerika. Serikali hii ikapambana na kundi la Al Shabab lililozalikana na muungano wa mahakama za Kiislamu ambao tayari ulikuwa

*Endelea Uk..6*


umepasuka na kuwa vikundi kadhaa.

Raisi huyu mpya aliyechaguliwa anakuja huku maafa yanazidi kuikumba nchi hii ya Somalia ilioko kwenye mahala pazuri pa kistratejia kwani inapakana na bahari ya Hindi na kuwa na ufuo mrefu wenye maili 1,700 sawa na kilomita 2,720. Kwa sasa taifa hili linakumbwa na baa la njaa linalohatarisha maisha ya zaidi ya raia milioni 5. Kuna na tatizo la ukimbizi ambalo vile vile maisha ya wakimbizi wa Kisomali wapatao milioni 5 yamo hatarini kufuatia jaribio la serikali ya Kenya ikiungwa mkono na Umoja wa Mataifa kutaka kuifunga kambi kubwa ya Daadab. Bila shaka matatizo haya yataendelea kuikumba Somalia licha ya kuchaguliwa serikali hii mpya ya kibaraka.
Kama alivyokuwa mtangulizi wake Hassan Sheikh Mahmoud, Farmanjo ataendelea kurithi na kutekeleza mipango ileile miouvu ya kikoloni iliyokuwa tayari imewekwa na mataifa ya Kimagharibi hasa Marekani. Matamshi yake ‘ ushindi huu unawakilisha maslahi ya wasomali…. ushindi huu ni wa Wasomali na huu ndio mwanzo wa kipindi cha muungano, Demokrasia na mwanzo wa kupambana na ufisadi’ Kwa maneno Farmanjo wazi ana wadanganya Umma wa Kiislamu wote na hasa Waislamu wa Kisomali kwani yeye binafsi alikuzwa na kufinyangwa na Amerika kwa lengo la kumakinisha ajenda mbovo za Marekani dhidi ya Somalia. Ni jambo linalotambulika kuwa nchini ya kisingizio cha kupambana na Ugaidi; Marekani na washirika wake wanaendelea kupora utajiri wa Somalia.

Somalia kama zilivyo biladi nyengine za Kiislamu itaendelea kukumbwa na matatizo mengi yanayotokamana na utiifu wa viongozi wa Kiislamu kwa mabwana zao wa Kimagharibi. Mizozo mingi ilioko katika Ulimwengu wa Kiislamu moja kwa moja chanzo chake ni uingiliaji wa mataifa ya kimagharibi na athari zao. Kwa kuwa Ulimwengu wa Kiislamu unaongozwa na viongozi vibaraka wa wamagharibi basi Umma upo katika maafa makubwa. Na kwa kuwa hakuna Khilafah – serikali huru basi maafa nchini Somalia na biladi nyengine za Kiislamu yatazidi.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Kuukumbatia Mfumo Wa Kirasilimali Ni Kama Kujidunga Mwiba



Husikika malalamishi mengi kutoka pembe zote duniani kuhusu kudhalilishwa na kunyanyaswa kwa wanawake. Wengi hujitokeza kuzungumzia mwanamke mara husemwa anatumiwa vibaya kwa kufanywa mtumwa wa nyumbani na mara anadhulumiwa haki zake. Haikuishia tu misemo bali kukaundwa tume mbali mbali za kuweza kumtetea na ati kumkomboa huyu mwanamke chini ya kauli mbiu ‘haki za mwanamke’. Mbali na haya, kuawekwa tarehe maalumu duniani nayo ni tarehe 8 Mwezi March kila mwaka ijulikanayo siku ya wanawake. Kwenye siku hiyo makongamano huandaliwa kuzungumzia Mwanamke. Mara nyingi huambiwa kuwa lazima mwanamke apewe nafasi ya kisiasa na kiuchumi na kadhalika hivyo akapewa mpaka nafasi katika serikali kinyume na ilivyokuwa hapo awali.Licha ya tume hizi nyingi na nafasi waliopewa ya kuwa na wawakilishi wao katika serikali,malalamishi haya bado ni yenye kuendelea.

Matatizo yanayomkumba mwanamke ni kwa kukosa kwake fadhila,mwanamke amekuwa mwizi wa fadhla.Ni matatizo haya haya aliyopata mwanamke katika zama za kijahilia,idhilali hizi hizi aliweza kupitia mwanamke kutoka kwa wanaume na jamii kwa jumla.Mwanamke aliteswa kuteswa na Majahili.Lakini Mtume (SAW) alipokuja na nuru (Uislamu) katika jamii,nuru iling’aa sana kwa mwanamke na kutoka katika giza la idhilalai lililokuwa limemgubika.

Fikra matata “Gender equality” –usawa wa kijinsia ati mwanamke ni sawa na mwanaume hupigiwa mnada na wamagharibi na wanawake wengi wameinunua. Fikra hii humaanisha kuwa mwanamke asiwe na mipaka katika mambo yake ashindane na mwanaume kwa kupigania ngazi za utawala, afanye kazi na kadhalika. Kulingana na mfumo wetu wa Uislamu ni kuwa ameweka wazi majukumu ambayo jinsia zote hutekeleza kama waja wa MwenyeziMungu pasina na kuangalia ujinsia. Mwanamke anawajibika kuswali, kutoa zaka, kuhiji na kufanya daawa kama inavyowajibika kwa mwanaume. Hata hivyo, kimaumbile Mwenyezimungu akamvua mwanamke kwa baadhi ya majukumu fulani kama uongozi hawezi mwanamke kuwa mtawala. Kulea watoto tokea kushika mimba, kunyonyesha na mfano wa hayo hizi ni hukumu maalumu kwa wanawake. Ama masuala ya kufanya kazi ni kuwa Uislamu hakumharamishia mwanamke lakini jukumu la kusimimamiwa malazi, lishe na nguo limetwikwa wanaume wa Kiislamu. Hivyo ndivyo Uislamu ulivyomlinda na kumuekea haki sahihi kulingana na maumbile yake.

Wanawake waliotutangulia walijifahamu wao ni kina nani,wanatoka wapi na ni wapi wanakoelekea.Walipotambua ni wapi wanapoelekea walijitahidi kujiandaa nako.Ndio maana baada ya kufwata sheria za Allah na Mtume saw hatukusikia tume yoyote imeundwa kwa ajili ya kumtetea mmwanamke haki zake.Walitoshekwa na sheria za Allah.Kinyume na Mwanamke leo,amezipuuza sheria za Allah na kujigubika katika giza totoro la utwaghuti. Giza ambalo hata kukawashwa taa ngapi”tume”,halitabadilika na kuwa nuru.

*Endelea Uk..7*


Email: uqab@hizb.or.ke

Wanawake wa sasa wamekuwa wezi wa fadhila,baada ya kukombolewa na kustiriwa na Uislamu,leo wanafanya mambo kinyume na Uislamu huo. Shida,dhiki na mateso ya ujahiliya yamemrudia huyu mwanamke,lakini ujahilia wa zama hizi na matazizo yake,mwanamke amejitakia.Ameona njia mbili na akaamua mwenyewe kufuata njia ya kombo na kuacha iliyonyooka akiiona kuwa ndefu sana,huenda ikamchelewesha katika safari yake au kutomfikisha kabisa.

Aidha wanawake wa zama hizi wameathiriwa na tamaduni mbovu za kimagharibi. Chini ya miito potofu ya kisekula kama vile 'my dress my choice' , uhuru wa kutangamana, pamoja na uhuru wa kibinafsi imewafanya wawawake leo kutojitambua wao ni kina nani,wanatoka wapi na wanakoelekea. Ama wale ambao kikusudi hawataki kujifunga na mafundisho bora ya Uislamu ndio urasilimali unawadhalilisha kiasi cha kutisha!

Kwa hakika thamani yake mwanamke inabaki kwenye vitabu na hadithi za bwana Mtume (saw) lakini thamani hii mwenyewe Mwanamke haitaki. Na hii ndio maana sisi kama wanawake wa Kiislamu, wanawake wa chama cha Hizb ut-Tahrir, ,tunasema dhiki hizi mwanamke zimesababishwa na kukubali kwetu kuishi chini ya fikra na mfumo hatari wa Kimagharibi wa kirasilimali. Lau hatutojifunga na Uislamu wetu basi ni mwiba wa kujidunga ambao siku zote pole huwa hauna. Tuna imani hakuna tume itakayoweza kumtetea mwanamke na kumuekea haki zake kama zilivyowekwa na Qur'an. Mwanamke aache kujidunisha na arudi katika Kitabu na Sunnah za Mtume (saw) na giza hili litapotea na watang'ariwa na jua na mwangaza wa Uislamu. Allah(swt) ametuonya kuwa mwenye kuacha utajo wake atampa maisha ya dhiki, mwanamke.

**Mgeni J. Salim**




# Urasilimali Hauwezi Tatua Shida Ya Ukosefu wa Ajira

Gazeti la Business Daily liliripoti mnamo Machi 9, 2016 kwamba Kenya, nchi kubwa kiuchumi kanda ya Afrika Mashariki, ina sifa mbovu ya kuwa nchi yenye idadi kubwa ya vijana wasiokuwa na ajira katika kanda hii. Ripoti rasmi ya Benki kuu ya Dunia iliyotolewa awali inaelezea kiwango cha ukosefu wa kazi Kenya – kwa sasa ni mara tatu ya majirani wake Uganda na Tanzania - pia ndio kiwango cha juu zaidi duniani. Ripoti inasema kuwa karibu kwenye vijana watano wa Kenya wa umri wa kufanya kazi mmoja hana kazi ikilinganishwa na Uganda na Tanzania ambapo mmoja katika kila vijana 20 ndio hawana ajira, ikisisitiza ukweli wa kiuchumi ambao vijana wa Kenya wanakabiliana nao. Ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana nchini Kenya sasa inakadiriwa kufikia asilimia17.3% ikilinganishwa na 6% kwa nchi za Uganda na Tanzania. Pamoja na Urasilimali kuchukuliwa kama ufumbuzi wa matatizo ya kiuchumi nchini Kenya, wimbi la kufungwa makampuni limegonga Kenya katika kipindi cha hivi karibuni na kuzua wasiwasi juu ya hali ya mazingira ya biashara nchini na duniani kwa ujumla. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Idara ya Kitaifa ya Takwimu, karibu kampuni milioni 2.2 za biashara ndogo zimefunga katika miaka mitano iliyopita. Ripoti hiyo, "Micro, Small and Medium Establishments", inasema nyingi ya biashara ambazo zimefungwa zilikuwa katika biashara ya jumla na rejareja kama vile kukarabati magari na pikipiki, sekta ambayo ilikuwa asilimia 73 ya jumla zilizofungwa. Idadi kubwa ya makampuni kufungwa ilikuwa katika mwaka wa 2015, ikiwa ni asilimia 35.4 ya jumla ya idadi ya makampuni yaliyofungwa katika miaka mitano iliyopita. Karibu kampuni milioni 1.2 zilifungwa katika maeneo ya vijijini ikilinganishwa na milioni moja katika maeneo ya mijini. ( Gazeti la The Standard Disemba 19, 2016)

Kama ilivyoripotiwa katika gazeti la Standard la Novemba 29, 2016, Benki ya Dunia mnamo Oktoba mwaka jana(2016) ilizindua ripoti ya Mazingira ya Kufanya Biashara ilioonyesha Kenya ilidhibiti nafasi yake ya tatu kama nchi iliyoboreshwa kimataifa. Lakini hata kama Serikali inafurahia mabilioni ya pesa yanayoingizwa katika uchumi na sifa inayopata kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara, mamia ya maelfu ya familia wanaangamia kwa kukosa ajira. Hiki ni kitendawili cha uchumi unaodaiwa kuwa kuongezeka kwa kiwango cha kuvutia, hata kama sekta ya kibinafsi – ambayo ni mzalishaji mkubwa wa ajira na mchangiaji wa kodi – inajitahidi ili kuendelea kufanya biashara. Tangu Januari 2016, zaidi ya kampuni ishirini zimefunga na kuhamia nje au kupunguza wafanyakazi zaidi ya elfu kumi. Sababu walizotoa ni ugumu wa mazingira ya kufanya biashara. Rushwa ni mojawapo ya vigezo ambavyo ripoti ya Benki ya Dunia juu ya urahisi wa kufanya biashara haiangalia wakati orodha yatayarishwa. Ikizingatiwa kwamba katika Kenya, rushwa ndio gharama kubwa ya kufanya biashara.

Endelea Uk..8

Baraza kutoka COTU anaamini kuwa ni kiwango cha juu cha ufisadi ndio chafukuza mashirika. "Ni ghali sana kufanya biashara nchini Kenya kwa sababu ni lazima kupeana rushwa kwa msururu wa watu binafsi. Lugha ya wafanyabiashara ni kwamba wanapunguza gharama, lakini uhalisi wa mambo ni kuwa hawezi kustahmili kiwango cha juu cha rushwa" akasema Baraza ambaye anasikitika kwamba Kenya imekuwa nchi ya maharamia. Kwa mujibu wa mwanauchumi David Ndii , Serikali kamwe haikuwezesha nafasi za ajira 824,000 mwaka 2015. "Sio kazi zinaundwa bali ni watu wanatengeneza ajira wenyewe," alisema Ndii.

Serikali ya Rais Uhuru Kenyatta iliahidi kuzalisha ajira mpya milioni moja kila mwaka kama sehemu ya ahadi za uchaguzi. Utawala wa Jubilee ambao kampeni yake kwa kiasi kikubwa ilikuwa kwa misingi ya kuwa timu ya ujana, pia iliahidi ukuaji wa uchumi wa kati ya asilimia 7 na 10 katika miaka miwili ya kwanza madarakani. Miaka miwili baadaye, uchumi ulizorota kutoka asilimia 5.7 mwaka wa 2013 hadi asilimia 5.3 katika mwaka 2014, kufuatia kushuka kwa biashara ya utalii na viwanda. Kwa bahati mbaya, tunachoshuhudia ni hadithi ya kusikitisha ya makampuni kufunga na kusababisha ukosefu wa kazi mkubwa. Kampuni ya East African Portland Cement ilitangaza kufuta wafanyakazi wake wapatao 1,000, Oserian Limitednayo mnamo Septemba ikasema itafurusha wafanyakazi 400 na Karuturi Flower Farm ilitimua wafanyakazi 2,600 baada ya kufunga kiwanda. Sameer Africa Limited ilitangaza kuwa itafunga kiwanda chake Nairobi baada ya mashindano makali kutoka matairi ya bei nafuu kutoka China na India. Kenya Fluorspar Company pia iliamua kusitisha shughuli za kikazi na kuacha watu zaidi ya 700 bila kazi. Eveready East Africa, ambayo ilifunga kiwanda chake cha Nakuru baada ya kulemewa kutokana na uagizaji wa bidhaa nafuu na hivyo kupunguza wafanyakazi zaidi ya 300. Pia wafanyakazi zaidi ya 200 wa Tata Chemicals walipoteza ajira katika kiwanda cha Magadi. Mashirika mengine yaliyoathirika ni pamoja na Colgate Palmolive, Reckitt Benckiser, Cadbury Kenya, Bridgestone, Devki Steel na Procter & Gamble ambayo yamebadilisha makao yao na kuhamia ugenini. Devki Steel ilifunga viwanda vyake nchini katika kile kilipelekea wafanyakazi takriban 2,000 kupoteza ajira. https://www.standardmedia.co.ke/business/article/2000193411/manufacturing-nightmare-that-is-turning-kenya-into-graveyard-for-companies

Benki pia hazikuachwa nyuma na baadhi ya wachambuzi walibainisha kuwa hii ni athari za utata wa Sheria za Benki mwaka 2016 ambayo iliweka kilele cha viwango vya riba na kupelekea kuwanyima wakopeshaji uhuru wa kutoza kodi ya juu ya viwango vya riba. Kile Serikali iliona kama chombo cha kuwezesha ushirikiano wa kifedha imegeuka na kuwa kidonge chungu kwa mamia ya wafanyakazi wa benki. Standard Chartered Bank iliwafuta wafanyakazi 167 kisha ikatangaza kwamba inasitisha kazi zisizo za msingi na kuzipeleka India katika hatua ambayo yatarajiwa kufanya wafanyakazi karibu 300 bila ajira. Family Bank pia wakajiunga kwenye msururu kwa kutoa fursa ya mpango wa hiari kustaafu mapema kwa wafanyakazi wake. Katika Januari 2016, Barclays Africa ilitangaza kwamba ilikuwa inafunga ofisi yake ya Nairobi na kuhamisha shughuli zake zote nchini Afrika Kusini. Haijabainika wazi kazi ngapi ziliweza kupotezwa. Equity Bank ikafichua kwa imewafuta wafanyakazi 400 katika kipindi cha miezi tisa hadi Septemba 2016, na kuendeleza mwenendo ambao ulianza mwaka 2015 wakati ajira 660 zilipotezwa kupitia mpango wa kuondoka kwa hiari. Ecobank ilikuwa pia imesema itawafuta kazi idadi isiyojulikana ya wafanyakazi kufuatia uamuzi wa kufunga matawi karibu 9 ya matawi yake 29 nchini Kenya. Na hii kwa hakika ni orodha finyu. Mamia ya makampuni mengine, hasa yale ambayo si ya ummah lazima yamefanya hivi mbali na jicho la vyombo vya habari.

Ukosefu wa ajira wa sasa na mgogoro wa kifedha ni dhihirisho la wazi la kushindwa kwa mfumo wa kibepari kushughulikia matatizo yanayowakabili wanadamu. Kenya ikiwa ni mfuasi wa mfumo wa kibepari, imeonyesha wazi kwa kila mtu kwamba maneno matupu hayatengenezi ajira bali ni mfumo unaotabikishwa ndio hukuza mazingira ya kuwa na ajira. Kazi ya serikali ya Kiislamu ni kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya biashara kustawi kwa kuondoa vikwazo vinavyozuia biashara kama leseni, rushwa, na ukosefu wa mtaji kwa kutoa mikopo isiyo ya riba nk. Kipaumbele kingine kwa Dola ya Kiislamu ni kuhakikisha kutosheleza mahitaji yote ya msingi (chakula, mavazi na makazi) kwa kila mwananchi. Mtume (SAW) alisema, "Mwana wa Adam hana haki bora zaidi ya awe na nyumba ambamo anaweza kuishi, kipande cha nguo ambapo anaweza kuficha uchi wake na kipande cha mkate na maji" [Tirmidhi] . Serikali ya Kiislamu ina wajibu wa kuangalia maslahi ya wale ambao hawawezi kujitosheleza ambayo inaweza kuwa imetokana na ukosefu wa ajira au ambao familia zao haziwezi kuwahudumia. Khalifah Umar bin Abdul-Aziz alimwandikia mwakilishi wake huko Basra, Iraq, 'Tafuta watu wa agano (dhimmi) katika eneo lako ambao wanaweza kuwa wamezeeka, na hawawezi kufanya kazi, na uwape marupurupu ya mara kwa mara kutoka hazina (Baitul Maal) ili kukidhi mahitaji yao [Al-Amwaal na Abu Ubayd: ukurasa 805].

Tunahitaji kuwakumbusha wote kwamba mfumo wa Kiislamu umekuja kwa ajili ya binadamu. Allah anasema:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ

**"Ni Sisi tumekutuma (Ewe Muhammad SAW) ili uwe ni Rehema kwa viumbe vyote." [TMQ 21: 107]**

Kwa vile ni mfumo kutoka Muumba wa wanadamu, ni sote tufanye kazi ili kurudisha upya mfumo huu tena.

**Kassim Agessa**
**Mwanachama katika Kamati ya Mawasiliano**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**



Email: uqab@hizb.or.ke